**Kiolezo cha Kongani la Kimataifa cha kudodosa taarifa muhimu kuhusu eneo la hifadhi ya jadi**

Asante sana kwa kujaza dodoso hili. Zingatia kuwa baadhi ya maswali yanaweza yasiwe muhimu kwa upande wako, hivyo hakuna shida ikiwa hutashughulika nayo au ukitoa majibu mafupi. Hata hivyo, majibu mengine ni muhimu kuyainisha.

*Kiolezo hiki kinaweza kupakuliwa kutoka toleo la tovuti la Mwongozo wa Mchakato wa Kujiimarisha wa Muungano wa Kongani la Kimataifa - pata maelezo zaidi kwenye* www.ssp.iccaconsortium.org

| | |
|---|---|
| JUMLA | |
| 1. | Tafadhali eleza jinsi ambavyo umekuwa ukidodosa kwa kutafuta uamuzi huru na wa hiari wa jamii/jamii ya wamiliki ili kutoa taarifa kuhusu eneo la hifadhi/matumizi ya jadi yaloiyojumuishwa katika taarifa ya Kongani na pia kuhusisha taarifa za mtandaoni (kulingana na maombi mahususi ya usiri au taarifa iliyodhibitiwa). |
| 2. | Je! Jamii ya wamiliki ni nani (k.m. jina na makadirio ya idadi ya wanachama, mtazamo wa idadi ya watu)? |
| 3. | Je, jamii inajitambulisha kama watu wa asili na/au ni ya watu wa kiitikadi au kabila dogo? (Kama ndiyo, ni watu gani maalum au maarufu?) |
| 4. | Ni lugha gani zinazozungumzwa katika jamii, zikiwemo lugha za wenyeji? |
| 5. | Ni watu gani wakuwasiliana nao muhimu katika eneo husika? Tafadhali jumuisha maelezo ya mawasiliano ya taasisi ya/za uongozi na/au mtu(watu) waliosaidia moja kwa moja kujaza dodoso hili. |
| 6. | Kwa lugha ya asili yao jina la eneo husika linajulikanaje (kwa lugha ya kitaifa au ya mkoa, inapofaa)? |
| 7. | Linapatikana wapi (nchi/mkoa/mkoa au jimbo)? |
| | KATI YA ENEO NA JAMII YA WAMILIKI NA MAADILI YA KIJAMII-UTAMADUNI. |
| 8. | Ni historia au msingi gani wa mahusiano ya jamii na eneo la hifadhi husika (k.m., utegemezi wa kuishi, utamaduni, uchumi wa ndani, fahari ya jamii, hisia ya utambulisho na eneo, hali ya kiimani)? |
| 9. | Eneo limewekewa mipaka na jamii? Kama ndiyo, ambatanisha ramani, ukibainisha 'ukanda' inavyowezekana. Eleza pia ikiwa 'eneo la hifadhi ya jadi' ni sehemu ndogo tu. |
| 10. | Ni maadili gani ya kidini **na shughuli** zinazohusiana na eneo husika? Ni eneo lote, au maeneo maalum tu, yanachukuliwa kuwa ya shughuli za kimila? Eleza. |
| 11. | Kuna ufahamu mzuri na wakutosha wa eneo na mazingira yaliyomo ndani yake? Onyesha ni kwa kiwango gani cha ufahamu na kama unatumika kikamilifu, jinsi ulivyoenea katika jamii, na kama unarithishwa kikamilifu katika vizazi vyote. |
| 12. | Wanaume na wanawake, wazee na vijana, au wataalam wa shughuli mbalimbali za kutafuta kipato cha kujikimu wanahusiana vipi na kwa njia gani na eneo husika? Je, wana maono tofauti katika suala la maadili ya kijamii na kitamaduni? Tafadhali eleza. |
| 13. | Kuna matukio yoyote maalum ambayo yanaimarisha utamaduni wa jamii na hisia ya utambulisho, mshikamano wa ndani na uhusiano na eneo la hifadhi (kwa mfano, sherehe, mila maalum au hija)? |
| TUNU ZA UHIFADHI WA MAZINGIRA | |
| 14. | Eneo la hifadhi ni kubwa kiasi gani? (eneo sahihi au makadirio katika hekta)? |
| 15. | Ni aina gani kuu ya mifumo ikolojia zilizomo ndani ya eneo (k.m., msitu wa ukanda wa juu milimani, msitu wa tropiki, milima, maji baridi, delta, uwanda wa nyasi, maeneo ya barafu yasiyo na miti, ncha ya kaskazini au kusini mwa dunia)? Inajumuisha eneo la bahari au maji baridi? Tafadhali eleza. |
| 16. | Ni aina gani ya mimea muhimu (pamoja zilizo hatarini, zilizo hatarini kutoweka au zilizo katika hatari kubwa ya kutoweka) na mahusiano yake makuu kiikolojia? Tafadhali orodhesha. |
| 17. | Eneo la hifadhi lina hali gani ya kimazingira (bora, nzuri, linatishiwa, mbaya)? Eleza kwa ufupi na uambatishe picha (ikiwa zinapatikana) na vichwa vya maneno, hatimiliki na ruhusa ya kutumia inayohitajika. |

| |
|---|
| 18. kwa kiasi gani na kwa njia zipi eneo la hifadhi ni 'nembo' na la kutia hamasa kwasababu ya mchango wake katika uhifadhi wa mazingira? (mfano, je, linasaidia aina mbalimbali ya mimea kuhifadhi wanyamapori au bioanuwai ya kilimo? Umuhimu kwa uwakilishi wa mfumo ikolojia, muunganisho wa uwanda wa maeneo mengine jirani kufanana, makazi ya kipekee, au ukanda wa mandhari za nchi kavu na mandhari ya bahari?) |
| 19. Serikali kwa njia yoyote ile 'imetambua' eneo lote au sehemu ya eneo hilo kuwa eneo lililohifadhiwa au imetoa utambuzi wa aina nyingine yoyote? Ikiwa ndivyo, je, jamii husika ilikubali kuhusu utambuzi huo au wa aina nyingine? Ilifanywa kwa ombi la jamii yenyewe au ilitambulishwa na wengine? (Ikiwa ni wengine, taja ikiwa ilifanywa na au bila uamuzi huru na wa hiari. |
| TUNU ZA KIPATO CHA KUJIKIMU KWA JAMII NA KITAIFA |
| 20. Ni kwa kiwango gani na kwa njia zipi eneo la hifadhi ni muhimu kwa kipato cha kujikimu kwa jamii (kwa mfano, chakula, maji, dawa,ujenzi, kipato, uhimilivu kutokana na majanga ya mazingira)? Je, jamii inashiriki kikamilifu, kwa wastani au kwa kiasi kidogo katika mnyororo wa soko la kiuchumi? |
| 21. Je, wastani wa pato la kila mtu ndani yajamii unalinganishwaje na wastani wa pato kitaifa (k.m., kidogo, takriban sawa au zaidi)? Je, mapato hayo yanategemea kwa kiasi gani eneo la hifadhi na utawala bora wa jamii husika? |
| 22. Ni kwa kiwango gani na kwa njia zipi eneo la hifadhi ni muhimu kiuchumi au vinginevyo kwa mkoa/jimbo au nchi (k.m., maliasili, maji, ulinzi, au kuzuia na kuhimili majanga ya kimazingira)? |
| UTAWALA NA HALI YA MAZINGIRA YA KISHERIA |
| 23. Je, kulikuwa na taasisi za jadi ambazo, kwa muda, zilitengeneza kanuni, desturi na maadili ambayo yamechangia kuwepo kwa eneo lahifadhi? Kama ndiyo, tafadhali eleza. |
| 24. Je, kuna taasisi maalum inayosimamia eneo husika leo (yaani, chombo kinachofanya maamuzi ya usimamizi na kuhakikisha kwamba maamuzi haya yanaheshimiwa)? Onyesha ikiwa ni taasisi ya kimila au ya kisheria au zote mbili/mchanganyiko; ikiwa ni pamoja na utaratibu wa kudhibiti migogoro na mabishano; na kama taasisi hiyo inaambatana na sheria za kimila au inahusiana nayo japo imeachana mila kiasi fulani. Tafadhali eleza. |
| 25. Je, taasisi hiyo (au jamii kwa ujumla) ina haki zozote za pamoja zinazotambuliwa na serikali au serikali ya kitaifa juu ya umiliki wa ardhi, maji na/au maliasili? Kama ndiyo, ni aina gani ya haki (k.m., umiliki wa kudumu, kutumia au kufikia, ukodishaji wa muda mrefu)? Je, jamii inahisi kuwa ina 'usalama wa umiliki' katika eneo husika? Tafadhali jadili. |
| 26. Je, kuna mwingiliano chanya au kinzani wa kisheria na sheria za kimila na taasisi za utawala? Kwa ujumla, jamii husika zinaonaje sheria zinazotumika katika eneo lao la hifadhi? Tafadhali eleza. |
| 27. Je, ni kwa kiwango gani na kwa njia zipi taasisi za utawala wa kimila au za mitaa huweka na kutekeleza sheria zilizo wazi na zinazojulikana za upatikanaji na usimamizi wa eneo la hifadhi ya jadi? Ni matumizi gani ya maliasili yanayoruhusiwa au kuzuiwa na jamii? Je, kuna matumizi tofauti yanayoruhusiwa katika maeneo au sehemu tofauti za eneo? |
| 28. Sheria hizi zinaratibiwaje na kupitishwa ndani ya jamii, kwa vizazi vijavyo na/au kwa washirika wa nje (k.m., kimaandishi au simulizi za mdomo, matambiko, itifaki za jamii, sheria ndogo ndogo, mipango ya ukanda)? |
| 29. Ni kwa kiwango gani na kwa njia gani jamii ina uwezo wa ndani wa kutumia teknolojia mpya (kama kompyuta, kamera za kielektroniki, Mfumo wa Kijiografia wa kuonyesha mahali, kuweka kumbukumbu na kuhifadhi taarifa), kuweka kumbukumbu na kuhifadhi taarifa, kusimamia rasilimali fedha, kuwasiliana kuhusu utawala na usimamizi wa eneo lake, nk. Tafadhali eleza |
| MATISHIO NA FURSA |
| 30. Ni matatizo/matishio gani makuu na fursa zinazokabiliwa na eneo husika, kwa mtazamo wa jamii na wamiliki? Zinahusiana kwa kiwango gani na kwa njia zipi moja kwa moja na eneo au jamii, wamiliki na taasisi inayoongoza? |

| | |
|---|---|
| 31. | Kuna mabadiliko yoyote makubwa au mienendo inayofanyika katika eneo husika (mfano, urejeshaji wa mfumo ikolojia, uhamaji au uhamiaji mkubwa, kupoteza au kuongezeka kwa mamlaka ya taasisi inayoongoza, masuala ya afya, ushiriki ulioimarishwa au hafifu wa vijana ndani ya jamii)? |
| 32. | Kuna migogoro mikubwa kuhusu umiliki wa ardhi, matumizi ya raslimali au mambo mengine kuhusu eneo? Tafadhali eleza, ikijumuisha fursa zozote za kuzishughulikia. |
| 33. | Kuna athari zinazoonekana za hali ya hewa au uharibifu wa mfumo ikolojia? Je, udhaifu mahususi unatabiriwa kutokana na hali ya hewa na majanga mengine? |
| | MAJIBU YA JAMII NA VIPAUMBELE |
| 34. | Jamii inakumbuka hali ambazo imeweza kulinda eneo lake kutokana na mabadiliko makubwa ya uharibifu? Kama ndiyo, tafadhali eleza. |
| 35. | Ni kwa kiasi gani wanajamii wanafahamu na wanashiriki katika kushughulikia masuala muhimu yanayohusu eneo (k.m., matishio, migogoro, juhudi za uhifadhi, fursa za kutambuliwa na kuungwa mkono)? Tafadhali eleza. |
| 36. | Wanajamii wamejipanga na kwa mshikamano na taasisi yao inayosimamia eneo lao? Je, wako wazi kuhusu jinsi ambavyo wangependa kutambuliwa na kuungwa mkono kama wamiliki wa eneo lao? Tafadhali eleza. |
| 37. | Ni nini mustakabali unaotarajiwa wa eneo lao kwa mtazamo wa jamii ya wamiliki? |
| 38. | Ni yapi baadhi ya mahitaji ya kipaumbele ya kujiamulia kwa jamii ya wamiliki kuyafikia kwa wakati unaotarajiwa? |

Nyenzo za kiambatisho (ikiwa zinapatikana):
Picha zenye muonekano mzuri za eneo la hifadhi ya jadi na wamiliki wake pamoja na vielelezo vyovyote vya rekodi na filamu ambazo unaweza kuwa nazo

- Ramani zilizotajwa hapo juu
- Majina na viungo vya vitabu vyovyote vilivyochapishwa au majarida ambayo yanaelezea sifa za asili, kitamaduni na/au kijamii na kiuchumi za eneo la hifadhi ya jadi (ikiwa vipo).